

HALMASHAURI YA MJI WA IFAKARA



SHULE YA SEKONDARI IFAKARA

S.L.P 148

IFAKARA

Tarehe

Simu Na.

023- 2625023

0753046896

0652480163

Web site: www.ifakara.sc.tz

Email - Ifakara.sec@gmail.com

Kumb. Na. ISS/SAG/23

Jina la mwanafunzi.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IFAKARA 2018 – 2019.

1. Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Ifakara kidato cha tano mwaka 2018 – 2019. Kwa michepuo ifuatayo:-
CBA, CBG, PCB, PCM, EGM, HGE, HGK, HGL, HKL
2. Nachukua nafasi hii kukupongeza na kukukaribisha shuleni. Ni matumaini yangu kuwa utaitumia nafasi hii kwa manufaa yako na ya Taifa hili.

JINSI YA KUFIKA SHULENI

Shule hii ipo halmashauri ya mji wa Ifakara Wilayani Kilombero Mkoa wa Morogoro.

USAFIRI WA BASI

3. Kwa usafiri wa basi kama unatokea Morogoro shuka sehemu iitwayo **KIBAONI** (Kilometa 4.5 kabla ya kufika mjini ifakara ukitokea Mikumi).Kutoka Kibaoni kuelekea shuleni ni umbali wa kilometa 1.5
Usafiri toka **Kibaoni** mpaka shuleni ni Tshs 1500/=tu kwa kutumia Bodaboda.

USAFIRI WA TRENI

Ukitumia usafiri wa Treni la TAZARA ukitokea Dar es Salaam au mbeya shukia kituo Ifakara na hapo unaweza kutumia Bodaboda kwa Tshs 2000/= tu.

- 4.(a) Masomo yataanza tareheunatakiwakufika shuleni siku tatu kabla ili kuyazoea mazingira.
(b) Ukichelewa kufika wiki mbili mara baada ya siku ya kuripoti nafasi yako itajazwa na mwanafunzi mwingine.
5. Ukifika shuleni ni lazima uripoti ofisini kwa Makamu mkuu wa shule. Hakikisha kuwa unamwonyesha barua hii ya kujiunga na shule.
6. Kabla ya kuanza safari ya kuja shuleni hakikisha unajaza fomu zifuatazo:

a) FOMU ZA USAJILI

- Fomu hii utaijaza wewe ukishirikiana na mzazi/mlezi wako nyumbani sehemu ya namba ya shule uache wazi maana sehemu hii itajazwa shuleni baada ya kupewa namba ya shule.
- Hakikisha mzazi /mlezi anatia sahihi yake kwenye mstari wa mwisho ulioandikwa sahihi ya mzazi/mlezi.
- Usaili wa mwanafunzi utahitaji aje na results slip pamoja na cheti cha kuzaliwa.

b) FOMU YA URAIA WA WAZAZI (CITIZENSHIP STATUS OF PARENTS

Wewe pamoja na mzazi / mlezi mjazie fomu hii mahakamani au kwa anayehusika na viapo ambaye ataweka sahihi yake pamoja na muhuri wake.

(c) FOMU YA HOSPITALI (MEDICAL EXAMINATION FORM)

Unatakiwa kupimwa na Mganga Mkuu wa Wilaya ili kuhakikisha kama una afya nzuri na kukujazia fomu iliyoambatanishwa.

TANBIHI: Hakikisha fomu hii inajazwa na Mganga wa hospitali ya serikali.

MAHITAJI YA SHULE

A. SARE ZA SHULE:

Sare ya shule hii ni sketi rinda boksi kitambaa cha suti rangi ya damu ya mzee (maroon) sketi 2 za darasani na rangi ya bluu (darkblue) sketi 1 kwa ajili ya kazi za nje. Rangi ya hijab (kijuba) ni nyeupe isiyokua na nakshi wala urembo aina yoyote kwa waislamu tu. Rangi ya shati ni nyeupe (**tomato**) ya mikono mifupi kwa wakristu na (**tomato**) ya mikono mirefu kwa waislamu.

Ili kuondoa matatizo yanayoweza kujitokeza kwa mzazi/mlezi kumnunulia mwanafunzi sare zisizolingana na mahitaji ya shule, hususani katika aina ya kitambaa na mshono unashauriwa kumtafuatia sare hapa shule kwa maana huwa tunawatafutia sare hizo na fundi. Pia sare yetu ni shati na tisheti inaambatana na nembo ya shule hivyo ni muhimu kuzipata shuleni, kwa mchanganuo ufuatao.

| | | | |
|---|---|------------------------------|----------|
| Sketi 3 | @ | Tshs 17,000/= x 3 = 51,000/= | Wakristo |
| Sketi 3..... | @ | Tshs 19,000/= x 3 = 57,000/= | Waislamu |
| Shati 2 zenye nembo ya shule | @ | Tshs 11,000 x 2 = 22,000/= | Wakristo |
| Shati 2 za mikono mirefu zenye nembo ya shule | @ | Tshs 13,000 x 2 = 26,000/= | Waislamu |
| T-shirt 2 zenye nembo ya shule | @ | Tshs 10,000 x 2 = 20,000/= | Wote |
| Tai 1 | @ | Tshs 4,000/= | Wote |
| Sweta 1 | @ | Tshs 18,000/= | Wote |

SARE ZA SHULE: Jumla- Wakristo Tshs **115,000/=**
Waislamu Tshs **125,000/=**

Malipo yote yapitie NMB-Bank –Sare za shule Ifakara sekondari. A/c Na. 21602301860

(TANBIHI: NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI KABISA.)

B MAHITAJI MENGINE YA SARE ZA SHULE

- I. Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili.
- II. Soksi nyeupe (stockings) jozi mbili.
- III. Suruali bluu isiyobana mwili kwa ajili ya darasani wakati wa prepo usiku ili kuzuia mbu (Jeans).
- IV. Raba nyeusi kwa ajili ya michezo, Taulo na blanketi.
- V. Truksuit za michezo mbili rangi ya bluu .
- VI. Vitabu vya masomo ya taasusi husika.
- VII. Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi.
- VIII. Mashuka pair 2 light bluu, foronya 1, chandarua moja nyeupe.
- IX. Vyombo vya chakula mfano. sahani, bakuli, kijiko na kikombe, mshwaki na dawa ya meno.
Ndoo moja ndogo na kidumu cha lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa
- XI .Madaftari makubwa (Counter book) walau 10.
- X. Uje na bahasha ndogo 4 kwa ajili ya kumtumia mzazi wako matokeo ya mitihani kila muhula.
- XI. Uje na fedha za matumizi madogomadogo pamoja na nauli ya kurudia wakati wa likizo na kila mwanafunzi. anashauriwa kufungua akaunti yake benk. NMB au CRDB.
- XII. Uje na Hijab mbili (nyeupe) zenye maadili ya kiislamu, ya kushona isiyokua na nakshi wala urembo aina yoyote -Kwa waislaamu tu.

NB; Katika kuondoa asumbufu kwa upatikanaji wa baadhi ya mahitaji yanapatikana katika DUKA la shule, kama vile Truksuit za bluu kwa ajili ya michezo, Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi, Mashuka pair 2 light bluu, Chandarua moja nyeupe, Madaftari makubwa (counter book), Vyombo vya chakula n.k.

TAARIFA ZA MALIPO

Malipo yote yafanyike benk katika A/C husika kwa utaratibu ufuatao:

i. ADA

(RECURRENT ACCOUNT IFAKARA SECONDARY SCHOOL A/C Na. 21601100085 NMB IFAKARA
Kwa muhula Tshs 35,000/= au Kwa mwaka Tshs 70,000/=

ii. **MICHANGO MENGINE** (A/C Na. 21601100004 UZALISHAJI MALI IFAKARA
SEC. SCHOOL NMB IFAKARA.)

MICHANGO MENGINE

| | | |
|--|----------|-----------|
| Mchango wa dawati | 15,000/= | Kwa mwaka |
| Tahadhari (hairudishwi) | 5,000/= | Kwa mwaka |
| Mchango wa mahafali | 15,000/= | Kwa mwaka |
| Kukodi godoro | 10,000/= | Kwa mwaka |
| Matibabu | 20,000/= | Kwa mwaka |
| Taaluma | 20,000/= | Kwa mwaka |
| Ulinzi na upishi | 30,000/= | Kwa mwaka |
| Computer | 10,000/= | Kwa mwaka |
| Kitambulisho | 6,000/= | Mara moja |
| Ream | 10,000/= | Kwa mwaka |
| Passport size | 5,000/= | Mara moja |
| Jembe, Mpini, Reki, na vifaa vingine vya usafi | 25,000/= | Kwa mwaka |
| Dissecting kit (wanafunzi wa sayansi) | 15,000 | Kwa mwaka |
| Mchango wa matron | 10,000/= | Kwa mwaka |
| Ukarabati wa vitanda | 10,000/= | Kwa mwaka |

NB: JUMLA; Kwa wanafunzi wa sayansi - **206,000/=** Kwa mwaka
Kwa wanafunzi wa sanaa - **191,000/=** Kwa mwaka

Ili kufanikisha uendedhaji wa shughuli mbalimbali za kishule, michango ya shule inashauriwa kulipa mara moja kwa mwaka.

JUMLA YA MICHANGO YOTE

ADA: (Recurrent account ifakara secondary school a/c na. 21601100085.....70,000/=

MICHANGO MINGINE: (Uzalishaji mali Ifakara Sekndari a/c Na. 21601100004

SARE ZA SHULE: (Sare za shule Ifakara sekondari a/c Na. 21602301860 125,000/= Waislam / 110,000/= Wakristo

NB: MALIPO YOTE YAFANYIKE KATIKA AKAUNTI HUSIKA.

Hakikisha unaandika jina la mwanafunzi anayelipa malipo Ada, michango mingine , na sare za shule kwenye hati ya kuweka fedha (**bank pay in slip**) na umshauri karani wa fedha aandike jina hilo pia.

Mwanafunzi ajapo shule apeleke pay inslip hiyo kwa mhasibu wa shule.

ZINGATIA KUWA FEDHA TASILIMU HAZIPOKELEWI.

NB: Dissecting kit inalipwa kwa wanafunzi wa sayansi tu.

TANBIHI

Unashauriwa kuja uipate elimu hii ya sekondari bila kukosa kwa manufaa yako binafsi maishani na kwa manufaa ya Taifa hili kwa gharama zozote zile. Kama wewe mwenyewe wazazi wako wanapaswa kutafuta ufadhili wa shirika lolote, Halmashauri ya Wilaya, au mtu binafsi ili akulipie gharama hizo. Mzazi / mlezi anaweza kufika shuleni kwa maelezo zaidi juu ya swala hili

MWEZI MMOJA KABLA YA KUFUNGUA SHULE.

- Hakikisha kuwa mfadhili wako au Halmashauri inakupatia malipo hayo kabla ya muhula kuanza vinginevyo utarudishwa kufuata malipo haya.
- Kila mwanafunzi ni lazima achange gharama za matibabu ili kupata huduma katika zahanati ya shule na hospitali ya wilaya inapolazimu.

SHERIA ZA SHULE ZA JUMLA

Kila mwanafunzi analazimika kuzisoma sheria za shule mara tu afikapo shuleni na zifuatazo ni sheria za jumla. Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya dini katika dhehebu au dini husika.

(1) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuchangia vyombo vya chakula.

(2) Mwanafunzi haruhusiwi kuweka fedha kwa mfanyakazi au mwalimu isipokuwa kwa mhasibu wa shule tu.

3) Mwanafunzi akiharibu au kupoteza mali ya shule atalipa.

4) Mafuta yenye harufu kali,perfume/spray,poda,rangi za kucha na midomo,wanja,curl,nywele za bandia,mapambo kama bangili,herein,mikufu,culture n.k.havitakiwi kabisa shuleni.

5) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya biashara mabwenini au maeneo ya shule.

6) Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya dini katika dhehebu lake husika.

7) Mwanafunzi aheshimu kengele,awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa.

8) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote.

9) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wanafunzi wenzake,kuheshimu ukumbi wa mikutano,mahali pa chakula pamoja na ofisi za shule.

10) Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua,ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule.

11) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu popote bila kibali cha uongozi wa shule ili kuepuka upelekaji wa taarifa zisizo sahihi kwa wazazi au walezi.Mawasiliano yote yatafanywa kupitia walimu wa malezi kama vile SDC,BM au Matron.

- 12) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mazungumzo na ndugu/jamaa yake msikitini, kanisani, hospitalini au nje ya mazingira ya shule. Kama ndugu/jamaa huyo ana maagizo afike ofisini aonane na uongozi wa shule.
- 13) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, nyimbo zote rasmi kama vile wimbo wa Taifa, wimbo wa shule, Tanzania nakupenda kwa moyo wote na Tazama Ramaani. (Kila mwanafunzi anatakiwa ajue kuimba nyimbo hizi).
- 14) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi. (Mwanafunzi mgonjwa anapaswa kupumzika katika chumba maalum).
- 15) Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anaruhusiwa kumwomba ruhusa mwanafunzi kama kuna tatizo. Pia ndiye atakayekuja shuleni pindi mwanafunzi atakapopatikana na kosa la kinidhamu na si mtu mwingine yeyote.
- 16) Mwanafunzi anapaswa awepo ndani ya sare za shule muda wote awapo shuleni na akikutwa na sare zisizokuwa rasmi atachukuliwa hatua.
- 17) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalum.

MAKOSA YAFUATAYO YATAKUSABABISHIA USIMAMISHWE AU UFUKUZWE SHULE

- 1) Wizi (2) Uasherati na ushoga (3) Ubakaji (4) Kuolewa (5) Utoro
- 6) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya. (7) Kupiga au Kupigana
- 8) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (9) Kudharau bendera ya Taifa na kutokuimba wimbo wa Taifa
- 10) Kupata kutoa au kuharibu mimba (11) Kugoma adhabu
- 12) Kugoma, kuchochea na kuongoza vurugu, kuvuruga amani ya shule
- 13) Kulala nje ya shule bila ruhusa ya uongozi wa shule.
- 14) Kuingia na kushiriki kwenye vilabu vya pombe na nyumba za kulala wageni.
- 15) Kukaa na kulala bwenini wakati wa vipindi.
- 16) Kukataa kufanya mazoezi na mitihani.
- 17) Kumiliki simu ya mkononi au kukutwa na viambatanishi vyake, kama charger, betri, vocha, line n.k
- 18) Kumiliki kifaa chochote kama pasi, heater, n.k

NB Kama mwanao hawezi kuishi bila simu ya mkononi, basi hafai katika mazingira ya shule ya sekondari Ifakara na ni vema asifike kabisa shuleni maana atafukuzwa shule mara moja.

Ni matumaini yangu kuwa mzazi/mlezi wako atashirikiana nasi katika kukuongoza hadi ufanikiwe kuipata elimu ya sekondari ya juu ipasavyo.

.....
MAGRETH DUNCAN LISSA
MKUU WA SHULE

IFAKARA TOWNSHIP COUNCIL

SHULE YA SEKONDARI IFAKARA

FOMU YA KUANDIKISHA SHULE USAJILI

JINA KAMILI LA MWANAFUNZI Na. YA SHULE.....
 JINA LA BABA
 JINA LA MAMA.....
 DINI Catholic/ Anglican/Islam/Hindu/SDA/Pentekost/AIC/Lutheran/ etc.....
 JINSIA: Msichana/Mvulana.....
 TAREHE YA KUZALIWA.....
 JINA KAMILI LA BABA.....
 ANWANI KAMILI YA BABA.....
 KAZI YA BABA.....
 MTAA..... Na. YA SIMU YA BABA KAZINI.....
 Na. YA SIMU YA BABA NYUMBANI.....

UKIWA HUKAI NA MZAZI, ANDIKA ANWANI NA JINA LA MLEZI WAKO
 JINA KAMILI LA MLEZI.....
 ANWANI YA MLEZI.....
 JINA LA ANAYEKULIPIA ADA NA MICHANGO YA SHULE.....
 ANWANI YAKE.....

JINA LA SHULE YA SEKONDARI ULIOFANYIA MTHANI WAKO WA KIDATO CHA NNE

 IKIWA ULIAMISHIWA KUTOKA SHULE YA SEKONDARI NYINGINE, ANDIKA JINA NA
 ANWANI YA SHULE HIYO.....

MAJINA SITA YA NDUGU WATAKAORUHUSIWA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SIKU
 ZINAZORUHUSIWA NA KUFANYA NAE MAWASILIANO ENDAPO KUNA TATIZO LOLOTE.
 (Jaza hapa chini). Hakikisha umri na mahusiano wa ndugu huyo uwe na msaada katika malezi na maendeleo ya
 mwanafunzi.

| S/Na. | JINA | ANWANI | NAMBA YA SIMU | MAHUSIANO |
|-------|------|--------|---------------|-----------|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |

TAREHE.....
 SAHIHI YA MZAZI/MLEZI.....

IFAKARA SECONDARY SCHOOL

P.O. BOX 148,
IFAKARA
DATE.....

CITIZENSHIP STATUS OF PARENTS

1.....(MAGISTRATE) Certify

1. That both parents are citizens by birth

a) Name of Father.....

b) Date and place of Birth.....

c) Name of Mother.....

d) Date and place of Birth.....

2. That both parents are citizens by registration naturalization

a) Name of Father.....

Passport or Registration number.....

Issued at.....

b)Name of mother.....

Passport or Registration number.....

Issued at.....

c) One of the parents is citizen by birth or naturalization.

If by birth: name of

Father/Mother.....

Place of birth.....

Passport or registration number.....

Date issued.....

Nationality of the Non – Citizen Parent.....

(mention country)

DATE.....SIGN.....

IFFUCUAK STANO..... COURT MAGISTRATE

Bring this certificate dully filled

APENDIX 'A'
GOVERNMENT OF TANZANIA

PART A: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To: the Medical Officer From
.....
.....
.....
Mr/Mrs/Miss.....

(Name in full)

Please examine the above named as to his/ her physical and mental fitness for a full time\ Secondary/University Education. The examination should include the following ineligible in case of defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate ineligible for secondary education.

- 1. (a) Eyesight (e) Venereal Diseases
 - (b) Hearing (f) Leprosy
 - (c) Speech (g) Epilepsy
 - (d) Limbs
- II. Neuroses
III. Other serious Diseases
IV Pregnancy

DATE..... SIGNATURE.....
.....

PART B : MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a government officer)

I have examine the above – named and consider that she is physically fit/unfit and mentally Fit/unfit for a full time Secondary / University Education

- a) Eyesight.....
 - b) Hearing.....
 - c) Speech.....
 - d) Limbs.....
 - e) Venereal Diseases.....
 - f) Leprosy.....
 - g) Epilepsy.....
- II. NEUROSIS.....
III. OTHER DISEAASES.....
IV. PREGNANCY.....
- Date.....Signature.....Station.....
- Designation.....

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO IFAKARA

A: SEHEMU YA MWANAFUNZI

1) Mimi
Ninakubali / Sikubali kujiunga na shule ya Sekondari ya kilimo ya Ifakara katika kidato cha
na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kutiini na kufuata sheria zote za shule
zilizowekwa kwa kipindi chote cha shule.

2) (a) Anwani yangu ya kudumu ni (b) Anwani yangu ya muda ni
.....
.....
.....
Sahihi ya mwanafunzi Tarehe

B: SEHEMU YA MZAZI / MLEZI

1) Mimi
Nimekubali/ Sikubali mtoto wangu..... ajiunge na shule ya
Sekondari ya kilimo Ifakara kuanzia tarehe.....
Ninaahidi kumlipia malipo yote ya shule na kumpatia vitabu vyote atakavyotakiwa kuwa navyo
shuleni kama ilivyoagizwa.

2) Anwani yangu ya kudumu ni: Anwani yangu ya muda ni
.....
.....
.....
Sahihi ya Mzazi/Mlezi..... Tarehe
Namba ya simu.....

HITIMISHO

- Shule yetu ni ya kilimo, hivyo mwanao anatakiwa awe tayari kushiriki na kupenda masuala yanayohusiana na kilimo.
- Hakikisha mzazi au mlezi umesoma kwa umakini fomu hii na kujadiliana na mwanao utayari wake katika kuzingatia yaliyo tajwa kwenye fomu hii.
- Utunzaji wa mazingira, kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali na kushiriki shughuli zingine zenye kuhamasisha uzalendo kwa nchi yetu ni lazima ikiwemo kushiriki katika vikundi mbalimbali hapa shuleni mfano CLUB, PCCB, FEMA n.k.

(Tafadhali njoo na fomu hii ikiwa imejazwa unapokuja shuleni).

KARIBU SANA IFAKARA SEKONDARI

IFAKARA SECONDARY SCHOOL
A - LEVEL BOOKS REQUIREMENTS

GEOGRAPHY

1. Human and Economic Geography by Goh cheng Leong Gillian
2. Research Methodology by Kothari C.R
3. Practical geography by Prichard
4. Physical Geography in Diagrams and practical Geography for Africa by printchard, m(1984)

CHEMISTRY

Chand Organic

Inorganic

Physical

1. Mark, Dand Hermer, D.S (2012) Physical chemistry with General chemistry (2nd ed) Dar es salaam APE network.
2. Jaini S.K (1998) conceptual chemistry New Delhi S. chand and company ltd (class II and 12
3. Organ chemistry (chand)
4. In – organic chemistry (chand)

KISWAHILI

1. MASEBO JAd Nyangwine N, (2011) Nadharia ya Fasihi kidato cha 5 na 6 (Toleo jipya) N.N Publishers, Dsm
2. Masebo JA & Nyangwine N, (2010) Nadharia ya lugha Kiswahili 1, kidato cha 5 & 6 (silabasi mpya 2009) N.N Publisher Dsm Tz.
3. Masebo JA & Nyangwine N, (2008) Tahakiki Vitabu Teule vya fasihi, kidato cha 5 na 6. Uhakiki na maswali - Toleo jipya NN publisher Dar es salaam Tanzania.

GENERAL STUDIES

1. Kas, (2010) General Studies A supplementary Book For A level and Colleges CETA – Dsm.